# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# KURUGENZI YA MAWASILIANO YA RAIS IKULU

*Simu: 255-262961500/1*
*Nukushi: 255-262961502*
*Baruapepe : press@ikulu.go.tz*
*Tovuti : www.ikulu.go.tz*

*OFISI YA RAIS,*
*IKULU,*
*1 BARABARA YA JULIUS NYERERE,*
*CHAMWINO,*
*S.L.P 1102,*
*40400 DODOMA.*

*Dar es Salaam*
*26 Julai, 2023*

**TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI**

**RAIS SAMIA ASHIRIKI MKUTANO WA WAKUU WA NCHI ZA AFRIKA KUHUSU RASILIMALI WATU**

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan amezitaka Serikali barani Afrika kuunganisha nguvu na asasi za kiraia pamoja na sekta binafsi ili kufanya uwekezaji stahiki.

Rais Samia ametoa tamko hilo kwenye mkutano wa Wakuu wa Nchi za Afrika kuhusu rasilimali watu uliofanyika katika kituo cha mikutano cha kimataifa cha Julius Nyerere.

Aidha, Rais Samia amesema ni lazima uwekezaji katika rasilimali watu uanze tangu mtoto anapozaliwa kwa kuhakikisha upatikanaji wa lishe bora na chanjo stahiki ili kuondoa udumavu unaopunguza kiwango cha uelewa.

Vile vile, Rais Samia ameongeza kuwa ni lazima kuweka msingi mzuri wa elimu kwa kuwa na maandalizi mazuri ya elimu ya awali kwa ajili ya kuwaandaa watoto kimwili, kiakili, kijinsia, kiubunifu na kihisia.

Rais Samia pia amesisitiza kuwa ili elimu itoe matokeo chanya ni lazima kuwa na mitaala yenye kukidhi matakwa ya soko la ajira sambamba na teknolojia mpya itakayoleta mabadiliko katika sekta mbalimbali.

Mkutano huu umekutanisha viongozi mbalimbali barani Afrika wakiwemo Marais 6 kutoka Madagascar, São Tomé na Príncipe, Msumbiji, Sierra Leone, Kenya na Malawi.

Zuhura Yunus
Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu